# JE MUNGU ANAIPENDA ULIMWENGU KIASI YA KUIOKOA?

**“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa kipekee...”**

**-Yohana Mtakatifu 3:16, Bila shaka ndicho kifungu kilichotajwa zaidi katika Biblia.**

**Lakini kama Mungu anaipenda ulimwengu sana, mbona anaonekana kufanya machache kuiokoa?**

Ni mahubiri mangapi, unafikiria zimehubiriwa kuhusu Yohana 3:16? Ni mara ngapi katika kila mwaka umesikia kuhusu kifungu hiki?

Inaonekana  kwamba kifungu hiki hupatikana kwenye maeneo yaliyo wazi. Unaweza kuwa umekiona katika kibao sebuleni mwa rafiki yako. Na kwa kweli umewahi kupewa vijikaratasi na kifungu hiki kikionekana kwa maandishi makubwa.

Pia tunapata kifungu hiki kimetajwa kwenye vibandiko na vibao. Kibao kimoja, kwa mfano, kikisema “Yohana 3:16 yaieleza jinsi ilivyo!”

Na kwa kweli, Yohana 3:16 yaieleza jinsi ilivyo. Mungu anaipenda ulimwengu; Anaipenda kwa upendo ule wa dhati kuliko mafikirio ya mwanadamu.

Biblia inatuambia kwamba Bwana ni "mwenye fadhili na rehema" (Zaburi 111:4); na fadhili zake ni "kubwa hata mbinguni" (Zaburi 108:4), kumaanisha kwamba fadhili na rehema zake hazina kiwango.

Katika Zaburi 136, kifungu "kwa maana fadhili zake ni za milele" inapatikana mara zaidi ya 26. Kwa wanaisraeli alisema, "naam, nimekupenda kwa upendo wa milele" (Yeremia 31:3). Na katika agano jipya, anaitwa "Mungu wa upendo na amani" (2Wakorintho 13:11).

Upendo wake ni mkubwa sana, Yeye "hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9). Yeye hutaka "watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli." (1 Timotheo 2:4).

Kwa kweli, upendo wake ni kuu kama nguvu zake za milele. Rehema na fadhili zake, haziwezi kupimwa wala kufafanuliwa kamili na wanadamu.

Asili ya muumbaji wetu inaweza kujumuishwa kwa maneno matatau yalioandikwa na mtume Yohana: "Mungu ni upendo" (Yohana 4:8, 16).

Yohana hakumanisha kuwa Mungu ni zaida ya wazo njema. Au dhana zisizo za ulimwengu huu; alimaanisha kuwa ishara kuu ya Mungu ni upendo.

Lakini kama Mungu amejaa upendo na rehema, na anataka kuwaleta wanadamu katika toba na maarifa ya ukweli,  mbona ulimwengu haupati wokovu?

Mtu lazima akubali, ikiwa Mungu *anajaribu* sana kuokoa ulimwengu, yeye hafanyi kazi nzuri.

Tukizingatia hali ya ulimwengu ya kisasa – kuongezeka kwa uhalifu, utumizi wa mihadarati, ugaidi, laana ya ukimwi, mvutano wa rangi, uhalifu wa kila aina - tunaweza hitimisha kimantiki kuwa Mungu anashinda nguvu za uovu, ya kuwa anaiokoa ulimwengu?

Kila siku *maelfu* ya wanadamu hufa *bila wokovu*. *Mamilioni* bado hawajaskia hata jina la Yesu Kristo. Ambalo ndilo la kipekee, "hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

Tangu nyakati za Adamu hadi sasa, *mabilioni* wamekufa bila kuokolewa. Kwa kweli, kwa wale wanadamu wote walioishi na kufa, wengi wao hawakupata kuokolewa.

Je! Sasa wanateseka  jehanamu? Je! Wanasubiri "ufufuo wa hukumu"? Je Mungu mkuu – Mungu ambaye ni "upendo," ambaye rehema zake ni za milele, asiyetaka mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba na ukweli – kuwahukumu mabilioni

hawa katika ziwa la moto, na kuwatoa kwa matumaini yoyote ya wokovu?

Baadhi ya “wahubiri,” tukijumuisha wahuburi mashuhuri katika televisheni, wanaamini kuwa Mungu atabadilisha ulimwengu kwa ukristo katika idadi ya miaka elfu moja (Ufunuo 20) kufuatia marejeo ya pili ya Yesu Kristo – kwa hivyo inaonyesha Mungu ana uwezo wa kuleta ulimwengu kwa toba na mabadiliko. Ingawaje, wahubiri hawa wanadai kwamba mtu yeyote akufaye leo bila ya “kumpata Kristo” hana matumaini ya kupata wokovu.

Kama Mungu anaweza kubadilisha ulimwengu, mbona asiifanye sasa, badala ya kusuburi hadi kurudi kwake kristo? Je! Wokovu unatagemea sana wakati mtu anazaliwa? Na je, mabilioni waliokufa bila kuokolewa? Na kama Mungu aliwapenda sana mpaka akamtuma Yesu Kristo awafie, mbona hakuwapatia fursa ya wokovu ambayo anawapa wale walio hai nyakati hizi za milenia?

Kwa maneno mengine, Mungu mwenye fadhili, rehema na asiyetaka yoyote kupotea kumpatia kila mtu nafasi sawia ya uokovu?

**Dhana za kuvutia**

Ukienda kwenye Televisheni na kusema mbele ya mamilioni ya kwamba Mungu hapeani nafasi sawia, utavutia majibu makali kutoka kwa umati wa wakristo wanaokiri. Utajipata kuwa chombo cha maneno na mashtaka, kwa yeyote yule ambaye ana

msingi dhabiti ya Biblia na hana usadikisho yoyote ataghadhabika kwa pendekezo ya kuwa Mungu hapeani nafasi sawia katika uhusiano wake na binadamu.

Lakini, hebu tuitazame. Dhana za kitamaduni kuhusu kifo na maisha baada ya kifo, jinsi ilivyo fichuliwa na wahuburi wenye msingi *hazionyeshi Mungu aliye na usawa!*

Inavyoonekana, “orthodox” waprotestanti wote huamini kuwa watu wengi watazima vibaya katika miali ya moto wa kuzimu ya milele kwa sababu walishindwa “kupata wokovu” walipokuwa duniani – licha ya mungu kutowapa nafasi nzuri ya kuzaliwa nyakati ya milenia, wakati maovu yatashindwa na njia ya wokovu kuwekwa bayana.

Wengi mara nyingi huamini kwamba tangu nyakati za Adamu akifurushwa kotoka katika bustani ya Edeni hadi sasa, ni wachache tu kulinganishawa ambao wameona neema ya “ardhi ya utukufu”; lakini umati usiohesabika – mafamilia nzima, makabila, mainchi – wameenda “mahali pa kuhukumiwa” bila ya matumaini ya kupata kujua furaha ya maisha ya milele ambalo ndilo kusudi la kuumbwa kwa mwanadamu.

Baadhi ya wanadamu wana msimamo ya kwamba ni lazima “kumkubali Kristo” wakati wa maisha hii watapata wokovu. Ilhali wengine husema wale wote waaminiye kwa Mungu na wanaishi maisha yasiyo ya dhambi – hata kama ni washiriki wa ukristo,uyahudi, uislamu, au dini ingine yeyote – watehesabiwa miongoni mwa waliookoka.

Wengi waharibifu, wanaokataa mafunzo kuhusu “ukosefu wa maadili za kiroho,” huamini kwamba wakristo watakatifu pekee ndio watafufuka katika “ufufuo wa maisha,” wakati wengine wote watafufuka baada ya milenia katika “ufufuo wa hukumu.” Wale ambao watafufuka katika ufufuo wa hukumu wataishi maisha marefu ya kutosha kulia, kusaga meno, kupiga mayowe na kuomba msamaha kabla ya kuchomwa na kupotelea mbali.

Unaweza kuwa “umeokoka” au “umepotea,” wahubiri husema. Unapokufa, yote yamekwisha – unapata tuzo ya wokovu au mshahara wa dhambi.

Lakini swali bado lipo:  Je,ni vipi kuhusu mabilioni walioishi kabla ya Kristo kuja? Na je, ni vipi kuhusu mabilioni tangu nyakati za Kristo ambao hawakujua njia za uokovu? Watafufuka katika ufufuo wa *hukumu*? Na je, umati wote wa wayahudi, waislamu, wahindi na wabudha waloishi na kufa bila ya kumkubali Yesu Kristo kama mkombozi watapotea milele?

Ama, inaweza kuwa mapenzi na rehema ya muumba ni kubwa zaidi kiasi kwamba mabilioni ambao walifariki na kuishi bila ya kupata wokovu wataishi tena, watapatate maarifa ya ukweli wa Mungu na nafasi ya ukombozi?

Kabla ya kujibu, wacha tuzingatie swali kwa ufupi  kama kutokufa ni tabia ya kawaida kwa roho ya binadamu ama ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa wale wanaokuja kwake kupitia toba na imani.

**Watakatifu “kuvaa” kutokufa**

Wakristo wengi huamini Biblia hufunza dhana za “kutokufa wa kiroho,” na “roho” mara nyingi huponea kifo ya mwili. “Roho” ya watakatifu huenda mbinguni; na “roho” ya wasiookoka kuenda jehanamu – kulingani na wengi wa kiprotestanti.

Lakini ikiwa watakatifu wataenda mara moja kupokea tuzo baada ya kifo ya kimwili, mbona Mtume Paulo antueleza kwamba kama hakuna *ufufuo* wa wafu, hakuna tumaini?

Paulo aliandika, “ikiwa, kwa jinsi ya kibinadamu, nilipigana na hayawani wakali kule Efeso, nina faida gani, wasipofufuliwa wafu na tule, na tunywe, maana kesho tutakufa” (1Wakorintho 15:32).

Mtume aliendelea kusema: “Kwasababu Bwana mwenyewae atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza…” (1Wathesalonike 4:16-18):na tarumbeta zitalia, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.Maana sharti uharibikao uvae kutokuharibika,nao huu wa kufa uvae kutokufa,hapo ndipo itakuwa lile neno liloandikwa,mauti imemezwa kwa kushinda(Wakorintho 15:51-54)

Je ulitambua Paulo alisema watakatifu, wawe hai au wamekufa, wata “vaa” kutokufa? Na kama kutokufa inapaswa kuvaliwa basi hatuko katika hali ya kutokufa – kutokufa haiwezi kurithiwa.

Hatuelezwi tu, kutokufa inapaswa “kuvaliwa,” tunaambiwa lini itavaliwa. Watakatifu watavaa kutokufa “siku ya parapanda ya mwisho” – atakaporudi Yesu Kristo. Basi kifo itamezwa kwa ushindi.

Ikiwa watakatifu kwa kweli wataenda mbele ya Mungu Baba na Yesu Kristo wanapokufa – kwa maneno mengine, ikiwa maoni ya “orthodox” ya kuenda mbinguni ni kweli – basi kifo, ya wafu watakatifu, tayari imemezwa kwa ushindi.

Paulo aliandika, “Kama Adamu sote tutakufa, hata kwa Krist sote tutapewa uzima wa milele lakini kila mtu kwa mpangalio wake mwenyewe: Kristo kama matunda ya kwanza; baadaye wale ambao ni wa Kristo kwa kurejea kwake” (1 Wakorintho 15:23).

Kama wafu watakatifu wameendea kupokea tuzo zao za mbiguni basi tayari wamekwisha “pewa uzima.” Lakini Paulo hawachi nafasi ya “mafunzo” kuhusu “kuenda mbinguni,” kwani anasema kwa uwazi kwamba watakatifu watapata uzima wakati wa kurejea ya pili wa Kristo, ambalo bado haijafanyika.

Jinsi inavyoshtuwa wakristo kwa ujumla, Mtume Paulo hakuamini “kuenda mbinguni baada ya kifo.” Alifunza kwa uwazi kuwa watakatifu watatunukiwa maisha ya milele baada ya ufufuo wa kifo.

Ni wazi, basi, kuwa ufufuo kutoka kwa wafu ni ahadi kwa watakatifu. Lakini ni vipi kuhusu wafu wengine – mabilioni

ambao hawakuwa watakatifu wa kikiristo nyakati za maisha zao? Je, wataishi tena?

Kama ni hivyo, ni lini? Watafufuka kutoka kwa wafu Kristo atakaporejea? Ama Biblia inafunza kuwa mabilioni wasiookoka watafufuliwa katika ufufuo tofauti?

**Ufufuo wa hukumu**

Jinsi tulivyoona, Biblia inafunza kwa uwazi ya kwamba watakatifu watafufuka punde Kristo atakaporejea. Katika Agano Jipya, huu ufufuo unaitwa "ufufuo wa uzima" (Yohana 5:29), ni "ufufuo wa wenye haki" (Matendo 24:14,15), na "ufufuo wa kwanza" (Ufunuo 20:5).

Lakini, ni vipi kuhusu waliokufa na hawafufuki kumlaki Kristo atakaporejea? Nini itawatendekea?

Katika Danieli 12 tunasoma kuhusu aina mbili za ufufuo. Nabii anaandika; "Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele. Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyote milele na milele" (mstari wa 2,3).

Wacha kwanza tutambue nini kifungu hiki hakituelezi. Licha ya kutuambia kuwa "wengi… watafufuka," haituelezi ni *wangapi*. "Wengi inaweza maanisha maelfu wachache, ama inaweza maanisha kila mtu."

Ya pili, kifungu hiki hakituelezi iwapo aina hizi mbili za ufufuo zitatendeka kwa wakati moja ama kwa wakati tofauti. Ikijisimamia, mstari wa pili inaonekana kusema zitatendeka pamoja. Hata hivyo, maandiko hailazimishi ufasiri huu, kwa kuwa Danieli anazungumzia agizo la mwisho ya vitu na hajaribu kuwasilisha mpangilio ya matukio ya "eschatological."

Na ya mwisho, hatuelezwi kama wale watakaofufuka katika aina ya pili ya ufufuo wataangamizwa ghafla ama kuna kipindi cha kuingilia kati, kati ya saa wanapofufuka na mwanzo wa "chukizo ya milele."

Tunaambiwa kwamba kuna aina mbili za ufufuo. Tunaweza kufikia hitimisho machache kwenye hiki kifungu.

Sasa, twende kwa Agano Jipya, na tuone kile Yesu kristo alisema kuhusu ufufuo.

"Msistaajabie maneno hayo" Yesu alisema, "kwa maana saa yaja, ambayo watu wengi waliomo makaburini wataisikia sauti yake na watatoka: wale waliofanya mema kwa *ufufuo wa uzima*; na wale waliotenda mabaya kwa *ufufuo wa hukumu*." (Yohana 5:28,29)

Tazama, Yesu anasema kwamba wote walio makaburini watakuja mbele zake. "Wote" kwa hakika inamaanisha zaidi ya wachache. Bila shaka inajumuisha mabilioni walioishi na kufa chini ya miaka zilizopita. Yesu anasema kuwa wote wataishi tena, kuwa watafufuka kupitia mojawapo ya aina hizi mbili za ufufuo – Ufufuo wa uzima au ufufuo wa hukumu.

Ni wazi, ufufuo wa uzima ndio ufufuo wa watakatifu, kitakacho tendeka Yesu Kristo atakaporejea. Lakini ni vipi kuhusu ufufuo wa hukumu; itatatendeka lini?

Maneno ya kifungu inaonekana kupendekeza kuwa aina zote mbili za ufufuo zitatendeka kwa wakati moja. Yesu alisema, "…Saa yaja, wafu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake." Hii inaonekana kusema ufufuo zote mbili zitatendeka kwa wakati moja. Lakini basi, inaweza maanisha pia kuna wakati unakujia ufufuo moja, na kuna wakati (wakati tofauti) unakujia ufufuo mwingine.

Mtume Paulo pia anataja aina mbili za ufufuo. Anasema "…ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio na haki pia" (Matendo 24:15).

Tena hatujapewa habari nyingi. Ni wazi kwamba ufufuo "ya walio na haki" ni sawa na "ufufuo ya uzima" ambaye Yesu alizungumzia, na ufufuo wa "wasio na haki" na "ufufuo wa hukumu" ni sawa, lakini maandishi ya Paulo haiku wazi. Je, anasema walio na haki na wasio na haki watafufuka kwa ufufuo moja? Ama aliamini kwamba aina hizi mbili za ufufuo zilipaswa kutengwa na kipindi cha kuingilia kati?

Kufikia sasa tumeambiwa kwamba kutakuwa na ufufuo wa kutokufa na ufufuo wa hukumu. Ya kwanza itahusisha wale "waliotenda mema"; na ya pili itahusisha waliotenda "maovu." Na wote waliomo makaburini, Yesu anasema, watafufuka kwa aina moja au nyingine.

Lakini hakuna vifungu vyovyote tulivyochunguza vimetueleza mengi kuhusu vipengele vya wakati zinazohusika katika ufufuo hizi.

Tusome Ufunuo 20, na tuweze kugundua kitu ambacho hatujaelezwa katika vifungu vingine.

Yohana anasema: "Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya uso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala na Kristo miaka elfu." (Ufunuo 20:4).

Watakatifu ambao wametoa maisha yao katika mauaji ya imani wanaonekana *wakiishi* na *kutawala* na Kristo. Ni wazi, hii ni maelezo ya ufufuo wa uzima. Yohana anasema: "…Huu ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wakristo, nao watatawale naye hio miaka elfu." (Ufunuo 20: 5,6).

Sehemu ya kwanza ya msitari ya 5 inatueleza "hao watu waliosalia hawakuwa hai, hata itimiye ile mwaka elfu moja." Maelezo ya Yohana kuhusu ufufuo baada ya milenia inapatikana mwanzo wa msitari wa 12; "Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama katika kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni

cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.”

Angalia, wale wanaofufuka katika ufufuo wa baada ya milenia *watahukumiwa*. Kwa  uwazi, hii ni *ufufuo wa hukumu*.

Na mwisho, tunapata aina hizi mbili za ufufuo – ufufuo wa uzima na ufufuo wa hukumu – zimetengana kwa kipindi cha miaka elfu moja.

Yohana anatuambia ya kwamba “wafu wengine” – wafu wote ambao hawakufufuka katika ufufuo wa kwanza – waliishi tena mwishoni mwa kipindi cha milenia. Kumbuka maneno ya Yesu “watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake.” Inaonekana kwa uwazi kwamba maelezo ya Yesu ama ya Yohana haimwachi yeyote nje – wafu wote ambao hawatafufuka katika ufufuo wa kwanza watafufuka katika ufufuo wa hukumu kufuatia milenia.

Lakini nini itafanyika katika “ufufo wa hukumu”? Wote waliofufuka katika ufufuo huu watatumbukizwa katika ziwa la moto? Je, watalia, watapiga mayowe, na kuomba msamaha kabla ya kuteketezwa na kutokomea?

## Siku ya mwisho ya hukumu ya milenia

Petro anaandika, “Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu,

maana hapendi mtu yoyote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9).

Kifungu hiki kinatuambia kwa uhakika kwamba Mungu hapendi mtu yeyote kukosa uzima wa milele. Msitari huu pekee inaharibu dhana ya kwamba wengine wanazaliwa ili wapotee.

Lakini hiyo sio yote. Kifungu hiki kinatupatia habari nyingine muhimu zaidi. Inatuambia ya kwamba wale ambao *watatubu* mbele ya Mungu *hawataangamia*. Hii ni jambo muhimu la kutilia maanani. Tafadhali kumbuka wakati tunazingatia mifano ya watu ambao labda walitubu mbele za Mungu au wale wangekuwa wameshuhudia miujiza na kazi za Yesu.

Mfano wa kwanza unapatikana katika kitabu cha Yona.

Wengi wetu tunajua hadithi hii. Mungu alimuamuru nabii wake Yona kwenda mji wa Ninawi "akapige kelele juu yake" (Yona 1:2). Lakini Yona alijaribu kutoroka "apate kujiepusha na uso wa Bwana" (Yona 1:3); Hakutaka kutimiza amri ya Mungu. Hata hivyo, Mungu alisisitiza kuwa Yona auchukue kazi, hivyo alitayarisha samaki mkubwa kummeza, na kumpeleka maeneo karibu na Ninawi, na kumtapika nje kwenye ardhi kavu.

Tuzingatie sura ya 3.

"Neno la Bwana lilimjia Yona mara ya pili kusema, ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa; ukahubiri habari nitakayo kuamuru. Basi Yona akaondoka akaenda Ninawi kama Bwana alivyonena. Basi Ninawi ulikuwa mji mkubwa mno, ukubwa

wake mwendo wa siku tatu. Yona akaanza kuuingia mji mwendo wa siku moja, akapaza sauti yake akasema, baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa" (mstari wa 1-4)

Yonah alihubiri habari aliopewa na Mungu. Hata alitaja masiku ya kutimiza unabii wake. "Baada ya siku arobaini, " nabii alilia, "Ninawi utaangamizwa!"

Lakini tazama kilichotokea:

"Basi watu wa Ninawi wakamsadiki Mungu; wakatangaza kufunga, wakajivika nguo za magunia, tangu yeye aliye mkubwa hata aliye mdogo." Habari ikamfikia mfalme wa Ninawi, naye akaondoka katika kiti chake cha enzi, akavua vazi lake, akajivika nguo za magunia na kuketi katika majivu. Naye akapiga mbiu, akatangaza habari katika mji wa Ninawi, kwa amri ya mfalme na wakuu wake; kusema, mwanadamu asionje kitu, wala mnyama, wala makundi ya ng'ombe, wala makundi ya kondoo; wasile wala wasinywe maji bali na wafunikiwe nguo za magunia, mwanadamu na mnyama pia, nao wakamlilia Mungu kwa nguvu, naam, na wageuke, kila mtu akaache njia yake mbaya na udhalimu ulio mikononi mwake. Ni nani ajuaye kwamba Mungu hatageuka na kughairi, na kuiacha hasira yake kali ili msiangamizwe?" (Yona 3:5-9).

"Mungu akaona matendo yao, ya kuwa wameiacha njia yao mbaya. Basi Mungu akalighahiri neno lile baya, ambalo alisema atawatenda; asilitende" (Yona 3:10).

Sasa, kumbuka kifungu kilichonukuliwa hapo awali. Mungu "hapendi mtu yeyote apotee bali wote wafikilie toba."

Watu wa Ninawi walitubu mbele ya Mungu! Walitubu wakiwa wamevaa magunia; walifunga, walimlilia Mungu kwa nguvu; sauti zao zilisikika mbinguni! Na Mungu alijibu kwa kuiokoa mji.

Watu waliokolewa kimwili lakini je, waliokolewa kiroho? Je, watakuwa katika ufufuo wa uzima? Watafufuka kutoka kwa makaburi zao kumlaki Kristo atakaporejea katika ufufuo wa kwanza?

La! Hawatamlaki! Hata kama walitubu maovu zao, watu wa Ninawi watafufuka katika ufufuo wa hukumu.

Wacha tuone ushahidi.

Yesu alisema, "Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosea; Kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona" (Mathayo 12:41).

Kwa uwazi, wana wa Ninawi wa kale ambao walitubu kupitia mahubiri ya Yonah watakuja wakati wa *ufufuo wa hukumu!* Hawatafufuka katika ufufuo wa uzima, ama ufufuo wa kwanza, hata kama walitubu, hawakupewa maarifa ya wokovu!

Laiti kama Yona angewahubiria njia ya wokovu, watu wa Ninawi – angalau wengi wao – wangekubali njia hiyo; wangepata wokovu.

Je, Mungu atahukumu watu wale waliotubu kwa kutowajibika kwa ujumbe ambayo hawakupokea? Je, Mungu mwenye upendo, rehema na fadhili na hataki yeyote kuangamia lakini wote waja kwa toba, kuwatupa hawa watu (waliotubu) katika ziwa la moto, mahali watateketea milele?

La sivyo!

Neno “hukumu” haimanishi “kukemewa”. Na ufufuo wa hukumu sio ufufuo wa kukemewa. Petro aliandika, “Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu…” (1 Petro 4:17). Kwa uwazi inatueleza Mungu anahukumu watu wake; anawapima kwa msingi wa kile wanachofanya na kile wanachojua. Kwa kweli haisemi kwamba hukumu lazima ianze nyumbani mwa Mungu.

Ufufuo wa hukumu, basi, sio wakati mabilioni ya watu wa nyakati za kale watafufuka kupatana na adhabu yao ya mwisho. Badala yake, ni wakati wa kupima. Na ili kupimwa kwa msingi, au kuhukumiwa, kutokana na vipengele vinavyohusiana na wokovu, inahitajika kwanza kupewa maarifa ya njia ya wokovu.

Biblia haionyeshi maelezo ya hukumu baada ya milenia, lakini picha za kipindi hicho hutoa ushahidi wa kutosha kwamba wokovu utapewa kwa wale ambao hawakupata nafasi ya kuokolewa.

Tazama Mathayo 11:21-24:

“Ole wako, korazani!” Ole wake Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidon, wangalitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko nyinyi.

Wakaazi wa Tiro na Sidoni hawakupata injili ya wokovu,hawakupata nafasi ya kuokolewa . Na wangeona kazi za ajabu za Yesu, wangetubu.Je,inawezekana ya kwamba Mungu mwenye rehema bila kipimo na fadhili atawakataza hawa watu nafasi ya uokovu.

La, hasha! Hata wanasodoma waovu watapewa nafasi kamili ya wokovu

Yesu alisema, “Nawe Kapernaumu, Je! Utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu; Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu” (Mathayo 11:23;24).

Wakaazi wa Sodoma walipatana na hatma ya kutisha – waliteketezwa hadi kifo. Mji wote uliharibiwa, na kupunguzwa kuwa majivu, wakati moto nan kiberiti vilipoanguka kutoka mbinguni (Mwanzo 19). Je, Mungu ana nia ya kufufua hawa watu kisha kuwateketeza *tena?* Ama, atawarudishia maisha yao kwa manufaa tofauti?

Fikiria kuihusu?  Malaika wawili waliotumwa na Mungu kule Sodoma (Mwanzo 19) wangefanya miujiza kama Yesu nyakati zake, *kungetokea toba*! Yesu alisema hivyo! Lakini watu wa Sodoma hawakuona uponyaji wa magonjwa, kutolewa kwa mapepo na hata kufufuliwa kwa wafu: hawakusikia injili ya Yesu Kristo. Siku ya hukumu baada ya milenia, wataelewa njia za wokovu, na, bila shaka watashuhudia kazi za kupendeza za mpendwa Mungu ambaye hapendi mtu yoyote kuangamia.

Je nini itatendeka wakati ujao wa hukumu? Wakati Biblia haionyeshi jinsi mambo yatafanyika wakati huo, tunaweza pata hitimisho kulingana na habari tulizopewa.

Kwanza, ni muhimu kugundua kwamba hukumu (hasaa pale wokovu inahusika) inahitajika maarifa. Kabla hatua ya hukumu kutendeka kikamilifu, mmoja lazima awe na hekima kuhusu njia ya wokovu na dhambi zake kibinafsi. Vipengele hivi viwili lazima viwe kabla ya toba kufanyika. Kwa hivyo, wakati watu wa Sodoma na Ninawi pamoja na mabilioni wengine, kufufuka kwa hukumu, watapewa hekima ya ukweli na wataletwa mbele ya dhambi zao.

Hata iwapo wataingia katika ufalme wa Mungu itategemea juu ya hatua ifuatayo. Mara tu Sodoma (na wengine) watajua ukweli, na mara tu wataona jinsi ni waouvu, iwapo watakataa kutubu watateketezwa katika ziwa la moto (Ufunuo 20:15).

Lakini wangapi wanaopewa ukweli wa Mungu, na nafasi ya kurithi uzima wa milele katika ufalme wake, watachagua kufa katika ziwa la moto?

Sauli wa Tarso bila huruma na kwa ukatili alitesa kanisa, "lakini Sauli, akizidi kutisha na kuanza kuwauwa wanafunzi wa Bwana" (Matendo 9:1). Alikiri kwa kifo chake Stefano (Matendo 8:1), na aliwatupa watu wa Mungu gerezani (Matendo 8:3). Bali, huyu mtu alitubu wakati Yesu Kristo alimpiga chini njiani akielekea Dameski (Matendo 9).

Ikiwa Sauli (aliyekua Mtume Paulo) alitubu na kuipenda jina alilolikemea, ni wangapi kati ya mabilioni wenye dhambi za kawaida kuazia miaka zilizopita wanaweza kukataa kutubu ikiwa Mungu atawafanyia jinsi alivyomfanyia Sauli?

Na ikiwa Mungu ni mtulivu, mwenye upendo, na mwenye huruma jinsi Biblia inavyosema – jinsi alivyo – basi kwa kweli mfano wa maonyesho ya mapenzi yake kwa Sauli, iliyosababisha wokovu wa Sauli, ni mfano wa upendo atadhihirisha kwa kila mtu.

**Mungu Hashindwi!**

Wahubiri hupaza sauti, "Mungu hatashindwa!" Kwa ushindi ataleta mataifa ya ulimwengu huu chini ya utiifu wake!" Wanatueleza ya kwamba sehemu ya ushindi ya Mungu itaonekana nyakati ya kurejea kwa "dhiki kuu," wakati maelfu

ya wayahudi watamrudia Kristo. Maandamano ya ushindi itaendelea, tunaelezwa, Kristo atakapoleta mamilioni kwa uongofu nyakati ya milenia.

Lakini ngoja, kama umati ya miaka zilizopita na mamilioni nyakati ya "dhiki kuu" watakuwa tayari wamepata nafasi zao za wokovu wakati Kristo atakapowasili, basi Mungu tayari ameshindwa!

Je! Mungu ni "mtaalamu"? Je, "anaheshimu watu"? Je anapendelea enzi moja ya historia ya binadamu juu ya ingine?

Mtume Paulo anasema, salio ya mabakio ya umati ya waisraeli ilipata wokovu. Aliandika, "Imekuwaje basi? Kitu kile ambacho Israeli alikuwa akitafuta hakulipata lakini wale waliochaguliwa (waliosalia) walikipata, na wengine walitiwa uzito. (Kulingana na maandishi Mungu aliwapa roho ya kulala, macho yasiyoona, na masikio zisizosikiza) mapaka siku hizi" (Warumi 11:7-8).

Paulo alitamani sana kwamba wenzake waisraeli wapate wokovu. Alikuwa tayari kujitosha hasara ya kibinafsi kwa wokovu wa ndugu zake. "Nasema kweli katika Kristo, Sisemi uwongo, dhamiri yangu ikinishuhudia katika roho mtakatifu, ya kwamba nina huzuni nyingi na maumivu yasiyokoma moyoni mwangu. Kwa maana ningeweza kuomba mimi mwenyewe niharimishwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, jamaa zangu kwa jinsi ya mwili" (Warumi 9:1-3).

Je, hii  inamaanisha  kuwa Paulo aliamini kwamba mamilioni ya Waisraeli ambao walishindwa kupata wokovu, ambao walipofishwa na Mungu, walipotea milele?

Mtume alisema, “Maana ikiwa kutupwa kwao (Waisraeli) kumeleta upatanisho kwa ulimwengu (Mataifa), Je! Kukubaliwa kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa?” (Warumi 11:15)

Baadaye, katika aya sawa, Paulo anaandika, “Hivyo israeli wote wataokoka” (Warumi 11:26).

Tazama, Waisraeli wasiobadilika watapata kutoka kwa Mungu “maisha kutoka kwa wafu” – kwa ufufuo – na “waisraeli wote wataokoka.”

Bila shaka, wataalamu watapinga. Kwao, Kifungu “maisha kutoka kwa wafu” inamaanisha kubadilika kwa ukristo, na haizuiliwi kwa maana hiyo: na “waisraeli wote” inamaanisha waisraeli 144000 wa nyakati za mwisho, na pia kwa yule mwana Israeli aliyebadilika wakati wa miaka iliyofuata.

Tena, tunajiuliza, Je Mungu ni mtaalau? Na ukombozi kwa ukubwa unategemea enzi mtu alizaliwa?

Paulo anaendelea kuandika: “Kwa maana kama nyinyi (Mataifa) zamani mlivyomwasi, lakini sasa mmepata rehema kwa kuasi kwao (Waisraeli): Kadhalika na hao wameasi sasa, ili kupata rehema kwenu wao nao wapate rehema. Maana Mungu

amewafunga wote pamoja katika kuasi ili awarehemu wote” (Warumi 11: 30-32).

Mpangilio wa Mungu kwa binadamu haiondowi yeyote, bila kujali jamii, nchi, ama enzi mtu alizaliwa.

Waovu wasioweza kuzingatiwa – waliokataa kutubu maovu yao, ambao hukataa kwa makusudi njia ya wokovu na kuchagua njia inayoelekea kwa kifo cha milele – wataharibiwa katika ziwa la moto. Bila shaka, hii itakuwa kwa wale wachache zaidi.

Ndio maana mtume Paulo aliandika, “Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wale njia zake hazitafutikani! Maana ni nani anayeijua nia ya Bwana? Au ni nani aliyekuwa mshauri wake? Au ni nani aliyempa yeye kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake. Utukufu una yeye milele. Amina” (Warumi 11:33-36)